

**NOVENA YA MEDALI YA MIUJIZA. ( Tarehe: 15 Nov.-23 Nov. 2021)**

Anza kwa kuibusu medali ya Miujiza kisha fanya ishara ya msalaba.

Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina



Nakuungamia Mungu Mwenyezi.....

Uje Roho Mtakatifu.....

**SALA YA NOVENA( ISALIWE SIKU ZOTE TISA )**

Ee Maria uliye safi na Bikira, Mama wa Bwana wetu Yesu Kristu na Mama yetu, tukiwa na matumaini makubwa kwa nguvu ya maombezi yako ya miujiza, sisi watoto wako wapendwa na waaminifu tunakuomba utupatie neema na fadhili tunazokuomba katika novena hii. Iwapo zitafaa kwa roho zetu na kwa roho za wale tunaowaombea (*taja ombi lako hapa*) Ee Mama Maria Bikira Safi, tupatie chuki kubwa ya dhambi, na usafi wa moyo utakaotuunganisha sisi na Mungu tu, ili kila wazo letu, neno na tendo letu yaongeze utukufu wake zaidi. Tupate pia roho ya sala na kitubio ili kwa njia ya kitubio tuweze kupata yale tuliyopoteza kwa dhambi. Mwisho tuweze kupata uzima wa milele kule ambako wewe ni Malkia wa Malaika na watakatifu. Amina

**Ee Maria uliyekingiwa dhambi ya asili utuombeee sisi tunaombilia ulinzi wako, na wale wote ambao hawaukimbilii ulinzi wako, hasa maadui wa Kanisa na waliokabidhiwa kwako. X3**

**Kwa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili wa medali ya Miujiza.**

Bikira Maria wa medali ya Miujiza, ninakutumainia kabisa wewe: ndiyo maana ninajiweka mbele yako kukuomba. Nakusih, uniokoe na mahangaiko haya, naomba mama wa medali ya miujiza uniombee neema ninazozihitaji. **Salaam Maria..**

Bikira Maria wa Medali ya Miujiza, naomba uniokoe kutokana na ndimi hizi za moto wa dhambi na kifo. **Salamu Maria**

Niombee Baraka, Bikira Maria wa Medali ya Miujiza na uwe tayari kuipokea sala yangu.

Naomba uniwezeshe kuwa na upendo mkubwa zaidi kwa Mwanao wa pekee, ili kila siku niweze

kufanya hija ya kumwenda Yeye, kwa kuniwezesha kuwa na neema ambayo ninakuomba sasa.

**Salam Maria**

**Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili wa Medali ya Miujiza, Utuombee**

**SALA YA KUMSIFU BIKIRA MARIA MKINGIWA DHAMBI YA ASILI**

Tumsifu Bikira Maria Mama wa Mungu, aliyekingiwa dhambi ya asili

Baba Yetu x1, Salam Maria x1, Atukuzwe Baba x1

Tumsifu Bikira Maria Mama wa Mungu, aliyekingiwa dhambi ya asili

Baba Yetu x1, Salam Maria x1, Atukuzwe Baba x1

Tumsifu Bikira Maria Mama wa Mungu, aliyekingiwa dhambi ya asili

Baba Yetu x1, Salam Maria x1, Atukuzwe Baba x1

**Tunakimbilia Ulinzi wako.....**

Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina

**WIMBO:**

**BIKIRA MARIA ULYEKINGIWA DHAMBI YA ASILI (J. Makoye)**

Bikira Maria uliyekingiwa dhambi ya asili, ee Mama/ utuombee sisi kwa mwanao (mpenzi) Yesu Kristu aliye mbinguni x2

1. Dhambi ya asili hukuipata, ili umzae mwana wa Mungu.
2. Wewe wasifiwa ulimwenguni, na Malaika wanakusifu
3. Kichwa cha shetani wakikanyaga, wewe ni mshindi wa hila zake.

*Avee Maria! Ulimwenguni kote wameungana kusali Novena hii. Karibu tuunganishe nguvu ya pamoja ulimwenguni kote, sote tuungane kwenye Moyo mmoja wa Mama Bikira Maria wa Medali ya Miujiza aliyezaliwa Bila dhambi ya Asili.*

*Kuletwa kwako na Fortunata Masaka chini ya Mwamvuli wa Rozari Hai Mtandaoni-Tanzania.*

*Tusali daima, tuombeane daima. Avee! Mapendo ni ya Milele. 0717-558222,*

[rozarihaitanzania@gmail.com](mailto:rozarihaitanzania@gmail.com), [www.rozarihai.or.tz](http://www.rozarihai.or.tz)